## HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA

**MUHT.FU.NA.10/2020/2021**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI TAREHE 12/11/2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1.Mhe.Belbara Makono | Diwani Ijanija | Mwenyekiti |
| 2.Bi.Leah Kibaki | Kaimu Mkurugenzi Mji | Katibu |
| 3.Mhe.Kapaya E.Sozy | Diwani Mbogwe | Mjumbe |
| 4.Mhe.Salim Abdulkadri | Diwani Nzega Mjini Mashariki | Mjumbe |
| 5.Mhe.Saada Abdallah | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 6.Mhe.Agness Kadama | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 7.Mhe.Nyelo.M.Kidaha | Diwani Mwanzoli | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA** –KWA TAARIFA

| | | |
|---|---|---|
| 1.Mhe.Hussein Bashe | Mbunge | Mjumbe |



Scanned with CamScanner

## WATAALAM WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ndg.Frank Chaki | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali watu |
| 2 | Ndg.Damas Mwakindingo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji ,Ardhi na Maliasili |
| 3 | Dkt.Jaspa Samwel | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 4 | Ndg.Ramadhani Omary | Mkuu wa Kitengo cha ukaguzi wa ndani |
| 5 | Ndg.Maulid Dege | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 6 | Ndg.John Mude | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 7 | Ndg.Khatibu Juma | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Udhibiti wa Taka Ngumu |
| 8 | Ndg.Felix Nyaulingo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji |
| 9 | Bi.Lovenear Welelo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 10 | Sekela Mmbelo | Kaimu Mganga Mkuu Mji |
| 11 | Ndg.Jocob Mwakalobo | Kaimu Mkuu Kitengo cha Manunuzi |
| 12 | Ndg.Godson Harry | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 13 | Ndg.Alfred Ntunga | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 14 | Ndg.Allen Meena | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 15 | Ndg.Amos Milanzi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 16 | Ndg.Geofrey Mwakanyamale | KNY:Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 17 | Bi.Nambua Semlugu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 18 | Ndg.Rocky Nguma | Afisa Biashara |
| 19 | Ndg.Atanas Mede | Afisa Mapato |
| 20 | Ndg.Lailejileji Daudi | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 21 | Ndg.Denis Kazinja | Mratibu TASAF |
| 22 | Bi.Lydia Eliah | Mratibu Ichf |
| 23 | Ndg.Enos Walwa | Afisa Malalamiko |

**SEKRETARIETI**

Wilbroad Chalambo - Mwandishi wa Vikao



Scanned with CamScanner

**MUHT.FU.NA.10/01/2020/2021 / KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 09:03 alasiri kwa salamu kisha aliwakaribisha wajumbe wajadili kwa umakini agenda zilizopo mezani.

**MUHT.FU.NA.10./02/2020/2021/KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 12.11.2021**

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo zijadiliwe katika kikao hiki:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao cha tarehe 12.11.2021
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 21/09/2021
4. Taarifa ya mapato na matumizi mwezi Septemba, 2021
5. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021
6. Taarifa ya Kitengo cha Manunuzi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021
7. Taarifa ya Kitengo cha Ukaguzi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021
8. Taarifa Idara ya Utawala kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba,2021
9. Taarifa ya Kitengo cha kesi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021
10. Taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Udhibiti wa Vihatarishi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021
11. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs.700,000,000.00 kupitia fedha za mfuko wa COVID -19
12. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs.250,000,000.00 kupitia fedha za mfuko wa tozo za miamala
13. Taarifa ya ununuzi wa mashine ya kufyatulia tofali
14. Ufafanuzi wa ulipaji wa kodi ya zuio kwa mafundi wenye vitambulisho vya ujasiriamali
15. Mengineyo
16. Kufunga kikao



Scanned with CamScanner

Septemba 2021 jumla ya kiasi cha TZS 2,671,471,500.00 kimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kiasi cha TZS 2,434,738,000.00 zikiwa ni fedha kwa ajili ya mishahara na TZS 236,733,500.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**1.3 RUZUKU YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO**

Kwa mwezi Septemba 2021, kiasi cha TZS 20,000,000.00 kimehamishwa katika akaunti ya Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Mapato ya ndani sawa na asilimia 35.00

Kuanzia mwezi Julai-Septemba 2021 Jumla ya kiasi cha TZS 104,500,000.00 kimehamishiwa katika akaunti ya Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na mapato ya ndani sawa na 56.68% ya mapato halisi (40%).

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo ya Fedha za ruzuku kwa mwezi Septemba, 2021 Halmashauri ilipokea kiasi cha TZS 105,465,167.63 kutoka Serikali Kuu na Wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.Halmashauri ya Mji wa Nzega katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilikisia kupokea ruzuku ya miradi ya Maendeleo jumla ya TZS 7,390,894,230.00 ambapo kwa kipindi cha Julai –Septemba 2021 jumla ya kiasi cha TZS 272,588,572.29 kilikuwa kimepokelewa sawa na asilimia 3.68.

**2: MATUMIZI.**

**2.1MATUMIZI MAENEO YASIYO YA RUZUKU**

Katika mwezi Septemba, 2021, Halmashauri ilitarajia kutumia kiasi cha TZS 143,064,105.00 kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani ambapo hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2021, kiasi cha TZS 122,592,072.51 kilikuwa kimetumika sawa na asilimia 85.69 ya lengo la mwezi, kuanzia Julai –Septemba 2021 jumla ya Kiasi cha TZS 239,846,872.51 kimetumika sawa na asilimia 9.46 ya lengo la mwaka ambalo ni TZS 2,535,902,781.75

**2.2 MATUMIZI MAENEO YA RUZUKU**

Kwa mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imetumia kiasi cha TZS 837,751,829.20 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Matumizi mengineyo na Mishahara) sawa na asilimia 89.97 ya lengo la mwezi..Kuanzai mwezi Julai -Septemba 2021 jumla ya kiasi cha TZS 2,501,149,767.20 kimetumika (Matumizi mengineyo na Mishahara) sawa na 23.07% ya lengo la mwaka ambalo ni TZS 10,841,802,000.00.



Scanned with CamScanner

## 2.3 MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO

Kwa upande wa Miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na mapato ya ndani jumla ya kiasi cha TZS 60,381,883.00 kimetumika kwa mwezi septemba, 2021.

Kwa upande wa Miradi ya maendeleo ya fedha za ruzuku jumla ya kiasi cha TZS 117,645,754.14 kilitumika kwa mwezi Septemba, 2021. Kuanzia mwezi Julai-Septemba jumla ya TZS 188,325,875.39 sawa na asilimia 2.4 ya lengo la mwaka ambalo ni TZS 7,862,637,258.67

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/05/2020/2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango , Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa mbele ya wajumbe ikieleza miradi iliyotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu, Mapato ya ndani ya Halmashauri na Wahisani mbalimbali kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/06/2020/2021 TAARIFA YA KITENGO CHA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ikiwa na Manunuzi yaliyofanyika katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/07/2020/2021 TAARIFA YA KITENGO CHA UKAGUZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa niaba Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ikiwa kama inavyoonekana hapa chini:-

| NO OF (QUERIES) FINDINGS ISSUED | NO. OF FINDINGS RESPONDED AND CLOSED. | NO. OF FINDINGS NOT RESPONDED | NO. OF FINDINGS UNDER IMPLEMENTATION | OVER TAKEN BY EVENTS. |
|---|---|---|---|---|
| **PREVIOUS QUERIES (FINDINGS)** | | | | |
| 69 | 10 | 00 | 39 | 19 |
| **CURRENT QUERIES( FINDINGS)** | | | | |
| 12 | 00 | 12 | 00 | 00 |
| **81** | **10** | **12** | **39** | **19** |



Scanned with CamScanner

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliyapitisha maoni ya kamati ya ukaguzi katika hoja ambazo zilikuwa zimesalia.

**MUHT.FU.NA.10/08/2020/2021 TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ikieleza kazi zilizotekelezwa na Idara kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/09/2020/2021 TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2021**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ikieleza kazi zilizotekelezwa na Idara kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/10/2020/2021 / TAARIFA YA VIHATARISHI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2021 IDARA NA VITENGO**

Mratibu wa Vihatarishi aliwasilisha taarifa ya Vihatarishi vya Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021 ikionyesha maeneo yenye vihatarishi na hatua za kudhibiti vihatarishi.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walikuwa na haya ya kujadili:-

**YALIYOJADILIWA**

Wajumbe waliuliza maana ya udhibiti wa vihatarishi na maeneo ambayo vinatokea.

Katibu alifafanua huu ni mfumo wa Serikali katika kudhibiti madhara/ hatari zinazoweza kujitokeza mahali pa kazi ili kuongeza ufanisi kiutendaji.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walishauri:-

**USHAURI**

Idara ya Mifugo ifuatilie mwenendo wa utekelezaji wa utoaji wa chanjo za mifugo vinavyotokea baada ng'ombe kupata chanjo.

**MUHT.FU.NA.10/11/2020/2021 / TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS.700, 000,000.00 KUPITIA FEDHA ZA MFUKO WA COVID -19**

Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs.700, 000,000.00 kupitia fedha za mfuko wa COVID -19 iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi ikieleza kuwa Halmashauri ilipokea fedha hizo mnamo tarehe 21 Oktoba, 2021 kutoka Serikali Kuu kupitia Mfuko wa UVIKO -19 kwa ajili ya ujenzi wa



Scanned with CamScanner

vyumba vya madarasa 20 katika shule ... fedha kiasi cha Tshs.300,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura(EMD) katika hospitali ya Mji wa Nzega.

Wajumbe walimpongeza Mheshimiwa Rais kutuletea fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe kwa kauli moja waliazimia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba 20 vya madarasa na ujenzi wa jengo la dharura (EMD) itumike njia ya 'force account' ili kuharakisha utekelezaji wa adhma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha vyumba vya madarasa vinakamilika mapema na kuanza kutumika baada ya shule kufunguliwa.

**MUHT.FU.NA.10/12/2020/2021 / TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 250, 000,000.00 KUPITIA FEDHA ZA MFUKO WA TOZO ZA MIAMALA**

Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs. 250, 000,000.00 kupitia fedha za mfuko wa tozo za Miamala iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi ikieleza kuwa Halmashauri ilipokea fedha hizo mnamo tarehe 21 Oktoba, 2021 kutoka Serikali Kuu kupitia Mfuko wa tozo za miamala kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Kitengwe kata ya Mwanzoli

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/13/2020/2021 /2021 TAARIFA YA UNUNUZI WA MASHINE YA KUFYATULIA TOFALI**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango , Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya ununuzi wa mashine ya kufyatulia tofali kwa kiasi cha Tshs.13,000,000.00

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipongeza Menejimenti kwa uamuzi wa kununua mashine itakayosaidia kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu.

**MUHT.FU.NA.10/14/2020/2021 / UFAFANUZI WA ULIPAJI WA KODI YA ZUIO KWA MAFUNDI WENYE VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi alisoma barua yenye Kumb.Na.TRA/RM/M/TGF/VOL.1/41/151 ya terehe 02 Novemba, 2021 kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa aliyoandikiwa Wakurugenzi wa Mkoa wa Tabora kuhusu ufafanuzi wa kodi ya zuio (Withholding Tax) kwa mafundi (Local fundi) wenye vitambulisho vya wajasiliamali wadogo wanaotekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi wa Madarasa , Zahanati na Vituo vya Afya.



Scanned with CamScanner

vyumba vya madarasa 20 katika shule 11 za Sekondari kiasi cha Tshs.400,000,000.00 na fedha kiasi cha Tshs.300,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura(EMD) katika hospitali ya Mji wa Nzega.

Wajumbe walimpongeza Mheshimiwa Rais kutuletea fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe kwa kauli moja waliazimia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba 20 vya madarasa na ujenzi wa jengo la dharura (EMD) itumike njia ya 'force account' ili kuharakisha utekelezaji wa adhma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha vyumba vya madarasa vinakamilika mapema na kuanza kutumika baada ya shule kufunguliwa.

**MUHT.FU.NA.10/12/2020/2021 / TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 250, 000,000.00 KUPITIA FEDHA ZA MFUKO WA TOZO ZA MIAMALA**

Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs. 250, 000,000.00 kupitia fedha za mfuko wa tozo za Miamala iliwasilishwa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi ikieleza kuwa Halmashauri ilipokea fedha hizo mnamo tarehe 21 Oktoba, 2021 kutoka Serikali Kuu kupitia Mfuko wa tozo za miamala kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Kitengwe kata ya Mwanzoli

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/13/2020/2021 /2021 TAARIFA YA UNUNUZI WA MASHINE YA KUFYATULIA TOFALI**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango , Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya ununuzi wa mashine ya kufyatulia tofali kwa kiasi cha Tshs.13,000,000.00

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipongeza Menejimenti kwa uamuzi wa kununua mashine itakayosaidia kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu.

**MUHT.FU.NA.10/14/2020/2021 / UFAFANUZI WA ULIPAJI WA KODI YA ZUIO KWA MAFUNDI WENYE VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara kwa niaba ya Mkurugenzi alisoma barua yenye Kumb.Na.TRA/RM/M/TGF/VOL.1/41/151 ya terehe 02 Novemba, 2021 kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa aliyoandikiwa Wakurugenzi wa Mkoa wa Tabora kuhusu ufafanuzi wa kodi ya zuio (Withholding Tax) kwa mafundi (Local fundi) wenye vitambulisho vya wajasiliamali wadogo wanaotekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi wa Madarasa , Zahanati na Vituo vya Afya.



Scanned with CamScanner

leleweke kwamba , Kodi inatozwa kwa mujibu wa Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 ambayo haijaeleza kwamba mafundi wenye vitambulisho vya Wajasiliamali wadogo kusamehewa kulipa Kodi ya Zuio. Kwa muktadha huo Mafundi hao wanapaswa kukatwa kodi ya Zuio kwa kufanya shughuli za Kitaalamu (Ujenzi).

Baada ya barua kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha.

**MUHT.FU.NA.10/15/2020/2021 /MENGINEYO**

Hapakuwa na mengineyo.

**MUHT.FU.NA.10/16/2020/2021/KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 10:04 jioni na kuwatakia wajumbe kazi njema.



Scanned with CamScanner

**UMEIDHINISHWA NA;**

**Jina** BELBARA MAKONO ............................ **Jina** SHIMARY MNDOLWA ............................

**Saini** ............................ **Saini** ............................

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**TAREHE** 26/11/2021 ............................



Scanned with CamScanner